**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 22/10/2021 CHA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI HADI SEPTEMBA, 2021) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**KUMB.NA.HW/KFUM/01/2021/2022 MAHUDHURIO**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Menas C. Komba | Diwani wa Kata ya Matimira | Mwenyekiti |
| 2. | Mh. Simon B. Kapinga | Diwani wa Kata ya Lilahi | M/M/kiti |
| 3. | Mh Monica Tamballah | Diwani wa Kata ya Maposeni | " |
| 4. | Mh. Philbert M. Soko | Diwani wa Kata ya Liganga | " |
| 5. | Mh. Manufred E . Mzuyu | Diwani wa Kata ya Muhukuru | " |
| 6. | Mh. Godfrey O. Komba | Diwani wa Kata ya Litisha | " |
| 7. | Mh. Filberta C. Luambano | Diwani wa Viti Maalum Litisha | " |
| 8. | Mh. George Ponera | Diwani wa Kata ya Magagula | |

**WATAALAM WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Neema M. Maghembe. | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 2. | Khashimu S. Lugome | Afisa Utumishi na Utawala (W) | Mtalaam |
| 3. | Stephen D. Mulisa | Mweka Hazina (W) | " |
| 4. | Andrew M. Macha | Afisa Biashara | " |
| 5. | Bumi J. Kasege | Afisa Elimu Sekondari (W) | " |
| 6. | Lucy S. Mbolu | Afisa Elimu Msingi (W) | " |
| 7. | Dkt. Erick Kahise | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) | " |
| 8. | Evergreen Mkongwa | Afisa Uchaguzi (W) | " |
| 9. | Bazil T. Mramba | Kaimu Afisa Manunuzi | " |
| 10. | John B. Mosha | Mkaguzi wa Ndani | " |
| 11. | Zosmo Nyirenda | Kaimu Afisa Sheria | " |
| 12. | Totnant Mwageni | Mdhibiti Ubora wa shule | " |
| 13. | Zawadi H. Nyoni | Kaimu Afisa Maendeleo ya jamii (W) | " |
| 14. | Zena Ibrahim | Afisa Mazingira na Uthibiti wa taka ngumu | " |
| 15. | Damian Luena | Afisa Ushirika | " |
| 16. | Nyange Athumani. | Afisa Mipango (W) | " |
| 17. | Charles S. Chavala | Mwandishi wa vikao | |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh.Jenista Mhagama | Mbunge wa Jimbo la Peramiho | Kwa Taarifa. |

**WATAALAM WASIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Zakayo Kaunda | Afisa Maliasili | Kwa Taarifa |
| 2. | Athumani Likungumwike | Kaimu Mhandisi wa ujenzi | " |

| | | |
|---|---|---|
| 3. David Kikasi | Kaimu Afisa Nyuki | Kwa Taarifa. |
| 4. Dkt. Geofrey Kihaule | Kaimu Mganga Mkuu | " |
| 5. John R. Luoga | Kaimu Afisa Tehama | " |
| 6. Hossana Ngunge | Mratibu wa TASAF | " |

**KUMB.NA.HW/KFUM/02/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliwakaribisha wajumbe na wataalam kwenye kikao cha kujadili taarifa za utekelezaji katika robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo aliomba ridhaa kutoka kwa wajumbe ili kikao kiweze kuendelea kulingana na kanuni za kuendesha vikao katika Halmashauri ambapo huishia saa 10.00 jioni, wajumbe walitoa ridhaa ya kuendelea na kikao ambacho kilichelewa kuanza kutokana na sababu zisizozuilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti aliwaasa wajumbe kujikita katika maeneo muhimu kutokana na kwamba wajumbe walishapitia makabrasha hivyo walitakiwa kwenda moja kwa moja kwenye agenda kwa ajili ya kupata ufafanuzi kutoka kwa wataalam.Kikao kilifunguliwa saa 10.13 jioni.

Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti alitoa hoja maalum ya kuhusiana na kikao kuchelewa kuanza jambo ambalo litapelekea wajumbe kushindwa kwenda nyumbani na kulazimika kulala nje ya Kata zao hivyo waliomba kulipwa posho ya kulala nje ya kituo cha Kata (Night allowance).

**KUMB.NA.HW/KFUM/03/2021/2022 KUTHIBITISHA AGENDA.**

Wajumbe walizipitia agenda zilizoandaliwa ambazo ni:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Mihutasari ya vikao vya Tarehe 13/09/2021 na 14/09/2021
4. Yatokanayo na KFUM cha Tarehe 13/09/2021
5. Kuwasilisha na kujadili taarifa za utekelezaji za robo ya kwanza (2021/2022)
    i. Taarifa za Utumishi na U tawala
    ii. Taarifa ya Mapato na Matumizi.
    iii. Taarifa ya Kitengo cha Manunuzi.
    iv. Taarifa ya Miradi ya Maendeleo.
    v. Taarifa ya Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.
    vi. Taarifa ya TASAF.
    vii. Taarifa ya Kitengo cha Tehama.
    viii. Taarifa ya Kitengo cha Sheria.
    ix. Taarifa ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo robo ya kwanza (2021/2022)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya kitengo cha Biashara kwa sasa inaingizwa kwenye Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira hivyo kuitenganisha na sehemu ya Idara ya Fedha na Biashara kama ilivyoainishwa katika Muundo wa Halmashauri ulioidhinishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu (MB) Mizengo Pinda mwaka 2011

Menejimenti inashauri taarifa ya kitengo cha Biashara iwe inaingizwa kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ili kuendana na Matakwa ya Kanuni Na. 43 (3) ya kanuni za kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Songea za mwaka 2019.

Afisa Utumishi na Utawala alitoa ufafanuzi wa taarifa hiyo ambapo Mheshimiwa Mwenyekiti alisema ni sawa taarifa ya Biashara kwenda Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wakati Taarifa ya Idara ya Maendeleo ya jamii ni lazima ipelekwe kwenye Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira.

Wajumbe walisema shughuli zote ni za Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambapo Mheshimiwa Mwenyekiti alisema utaratibu wa kufanya mabadiliko lazima yafuate utaratibu hivyo, mabadiliko yasifanyike kabla ya kupitia vikao. Taarifa ilipitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti alisema OTC Lilambo Mkodishwaji wa mashine mchakato uendelee.

**KUMB.NA.HW/KFUM/08/2021/2022 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KWA AJILI YA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI.**

Taarifa ziliwasilishwa na Afisa Elimu Msingi (Madarasa shule shikizi TZS 380,000,000.00) na Afisa Elimu Sekondari (Madarasa Sekondari **TZS 920,000,000.00**) ambapo kwa upande wa Elimu Msingi wajumbe walipongeza hatua ya Serikali kukamilisha ujenzi wa Madarasa ya shule shikizi na kwa upande wa Elimu Sekondari wajumbe walimtaadharisha Mhandisi wa ujenzi kuwa makini katika kusimamia fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti aliagiza ifikapo mwezi Disemba, 2021 Madarasa yawe yamekamilika na kwamba kutakuwa na maelekezo mahususi yatatolewa kwenye kikao cha kazi na BOQ zitolewe kwenye kikao hicho pamoja na hayo utapangwa utaratibu wa kutekeleza miradi hiyo ya kujenga madarasa.

Mkurugenzi Mtendaji aliwaambia wajumbe kwamba watendaji wa vijiji wote tayari wana taarifa kuhusiana na kikao hicho mahususi cha maelekezo sambamba na TARURA na RUWASA isipokuwa TANESCO alisema hawakupokea simu kwa ajili ya kikao hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti alisema kutakuwa na kikao mahususi cha maelekezo kwa wataalam kutoka taasisi mbalimbali ambacho kitaongozwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Songea kabla ya kuendelea na kikao cha kazi cha robo ya kwanza (2021/2022).Mheshimiwa Mwenyekiti aliwaasa waheshimiwa Madiwani kusimamia miradi hiyo ambapo aliwatadharisha fedha hizo ni za moto pia kuna fedha nyingi zina kuja. Taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.HW/KFUM/69/2020/2021 KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti aliwashukuru Mkurugenzi Mtendaji, waheshimiwa wajumbe, wataalam kwa kuweza kushiriki kikao kwa uvumilivu na kutoa michango yao ya mawazo. Aliwashukuru wataalam kwa kuweza kutoa ushirikiano kwa wakaguzi wa mahesabu wa nje ambao waraendelea na kazi ya ukaguzi kama ilivyo ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti alimsifu Mhandisi wa Ujenzi Ndugu Athumani Likungumwike kwa kufanya kazi vizuri pamoja na kwamba yuko peke yake lakini ameweza kumudu majukumu ya kazi yake vizuri kwa sababu kila sehemu ya Halmashauri inamtumia.Sambamba na wataalam wengine aliwapongeza kwa kufanya kazi vizuri mpaka watu wanawasifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti alimsifu Mkurugenzi Mtendaji kwa kushirikiana vizuri na wataalam wengine wa Halmashauri hadi Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Ruvuma imewapongeza kwa miradi ya maendeleo kwamba fedha zimekuwa zikitengwa na kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo zina usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti alisema miradi ya Elimu hususani miradi ya EP4R ndiyo iliyofanya vizuri hivyo alimuasa Afisa Elimu Msingi kuwashirikisha waratibu Elimu Kata (MEKs) kwa ajili ya kusimamia vizuri miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti alimuasa Afisa Habari kuhakikisha anaandika mahitaji kwa ajili ya kupata vitendea kazi kwa kushirikiana na watu wa kitengo cha Manunuzi na Ugavi, pia alimsifu Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa ushauri wake mzuri, kikao kilifungwa saa 3.48 usiku.

UMETHIBITISHWA

.................................... SAHIHI YA KATIBU

.................................... SAHIHI YA MWENYEKITI

TAREHE 11/11/2021............................